JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO

YA UFUNDI STADI

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

# MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 20 mwezi 01 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha VETA-MARA, S.L.P. 188, MUSOMA ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802 DODOMA (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

EDWARD J. MAREGESI S.L.P. 601, MUSOMA (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundi") kwa upande mwingine

**KWA KUWA** Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya BUTIAMA;

**KWA KUWA** Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya BUTIAMA;

**KWA KUWA** Mwajiri amefanya majadiliano na Fundi kwa ajili ya kazi ya KUFUNGA MIKANDA NA BOARDS (NYUMBA YA MKUU WA CHUO PAMOJA NA NYUMBA ZA WATUMISHI)

**NA KWA KUWA** Mwajiri amempatia Fundi nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi itakavyofanyika;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 350,000.00, Fundi atafanya kazi ya LAKI TATU NA NUSU kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu. Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (*CONTRACT SUM ADJUSTMENT*)

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

(a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
(b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundi;
(c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundi;
(d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya Ufundi;
(e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundi;na
(f) Baada ya kukamilika kwa"Muda wa matazamio":5% ya Gharama ya Ufundi.

4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI

(a) Fundi atakabidhiwa eneo la tarehe..20..... mwezi ..01... 2022 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.

(b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku....5.......toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.

(c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

5. WAJIBU WA FUNDI

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kujenga UFUNGAJI MIKANDA NA BOARD na kukamilisha ujenzi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Vifaavya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA VETA-MARA.

Jina: DAVID L. BENEDICT Saini: ____________

Wadhifa: Msimamizi wa Mradi Butiama DVTC Tarehe: 20.01.2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: ALFRED G KIDIFU Saini: ____________

Wadhifa: AFISA MANUNUZI Tarehe: 20/01/2022

IMESAINIWA NA FUNDI

Mbele ya

Jina: EDWARD JONAS MAREGESI Saini: ____________

Wadhifa: FUNDI MKUU Tarehe: 20/01/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: EDWIN LUCAS Saini: ____________

Wadhifa: SHAHIDI Tarehe: 20/01/2022